

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI



TAARIFA KWA UMMA

Kwa muda mrefu sasa pamejengeka tabia na mazoea ya wananchi kuvamia na kuanza kutumia ardhi inayomilikiwa na Serikali, taasisi mbalimbali au wananchi binafsi. Uvamizi huo hufanyika kwa matarajio kwamba baada ya muda Serikali itawahalalisha hao wavamizi kumiliki ardhi hiyo.

Wizara inatoa Taarifa kwa Umma kuwa kitendo cha kuvamia na kuanza kutumia ardhi usiyomilikishwa kisheria ni kinyume cha sheria za nchi. Tabia hiyo haiwezi kuvumiliwa kwa nchi inayofuata utawala wa sheria; hivyo kuanzia sasa wananchi watakaovamia ardhi inayomilikiwa kisheria watakuwa wanaondolewa bila kulipwa fidia na hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi yao.

Wizara inazielekeza Halmashauri zote nchini kuendelea kuchukua hatua dhidi ya wavamizi wa ardhi (mashamba, viwanja na maeneo ya wazi). Aidha, Wizara inawataarifu wananchi wote kuwa uvamizi wa ardhi ni kosa la jinai chini ya fungu la 177 (3) la Sheria ya Ardhi (Sura 113).

Imetolewa na:

KATIBU MKUU